

- Watenganishe wakubwa kwa wadogo ili kuzuia kupigana.
- Wakati wa kuwaachisha kunyonya mwondoe mama yao kutoka kwa watoto ili kupunguza shirikizo/usumbufu.
- Watoto wa nguruwe wa mama tofauti wasiwekwe pamoja maana hii husababisha vita na upungufu wa uzani.
- Unapowachanganya watoto wa mama tofauti wapake mafuta ya gari yaliyotumika kwenye ngozi yao ili kuiondoa harufu ya kutambulika.



**Kuimariswa kiwango cha kutokufa**



### **Kenya Agricultural Research Institute**

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax. 254-20-4183344

Baruaapepe: [resource.centre@kari.org](mailto:resource.centre@kari.org)

Tovuti: [www.kari.org](http://www.kari.org)

#### **Watayarishaji:**

Githinji M. G. na Waithera L

#### **Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:**

#### **Mkurugenzi wa Kituo,**

KARI-Naivasha

S.L.P. 25 Naivasha

Simu: 050 5050483


Nukulishi: 050 5050483

Baruaapepe: [kariaiv@kenyaweb.com](mailto:kariaiv@kenyaweb.com)

Vijitabu nya KARI nya taarifa, nambari / 46 /2008

**Shilingi 20 za Kenya**

# **Utunzaji wa nguruwe wachanga ili kuimariswa ufugaji wa nguruwe**



## Utangulizi

Vifo vya nguruwe wachanga hupunguza faida ya biashara ya nguruwe kwa kupunguza idadi ya nguruwe wazima wa kuuzwa.

Utzunaji mzuri wa nguruwe wachanga huepusha vifo vinavyotokana na shida kama:

### Matatizo ya kupumua

Ni kifo kinachosababishwa na mama anapomlilia nguruwe mchanga. Hii inaweza kupunguza kwa kujenga kibanda cha watoto. Nguruwe wa kuzaa wachaguliwe kwa makini wenye uwezo wa kuwalea watoto ili kuimarisha kiwango cha nguruwe wachanga wanaokua bila kufa.

### Baridi

Nguruwe wachanga huathiriwa na baridi sana haswa katika majuma ya mwanzo mawili au matatu. Hii ni kwa kuwa wana kiwango kidogo cha utando wa mafuta wa kuwakinga.



Nguruwe wachanga wanaoweza kuangamia haraka

Waweke katika hali ya joto, wape matandiko na utumie vipasha joto kama vile kuasha globu za joto.

### Mitindo wa utunzaji wa nguruwe wachanga

Nguruwe moja wa kike ana uwezo wa kuzaa watoto 12. Mitindo ifuatayo itasaidia kupunguza idadi ya vifo vya nguruwe wachanga:

- Nyunyizia dawa ya ayodini 5% kwenye kovu ili kuzuia kuambukizwa kwa magonjwa.
- Wawekee matandiko (nyasi kavu au maganda ya miti) mahali pa mapumziko ili wapate joto au utumie globu za joto.
- Wadunge sindano ya madini ya chuma (iron) siku ya tatu ili kuzuia upungufu wa damu.
- Yalainishe meno kabla ya masaa 24 ili kuzuia uharibifu wa matiti wakati wanaponyonya.
- Watie vibandiko au utoboe masikio ili uwatambue na uhifadhi rekodi zao.
- Wapime uzani wanapozaliwa na uhifadhi rekodi hiyo.
- Wahasi wale wa kiume juma la tatu, wale ambao hawafai katika kuendeleza kizazi kwa kutumia mtindo wazi (open method).




Njia wazi za kuhasi

- Wapatie dawa ya kuzuia minyoo.
- Waachishe kunyonya katika juma la nane au wafikapo kilo 14 hadi 20.

### Walioachishwa Kunyonya

Walioachishwa kunyonya wawekwe makundi ya 10 hadi 12 kulingana na uzito wao.



Nguruwe aliyeachishwa kunyonya mwenye afya